

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA**

MKOA WA NJOMBE

Anuani "Afya"
Nambari ya Simu +25526-2782912
Fax Na. +225 – 262782914
Email: njomberrh@afya.go.tz



Hospitali ya Rufaa ya Mkoa,
Mtaa wa Mgodechi,
S.L.P. 1044,
NJOMBE.

31/01/2022

Unapojibu Tafadhali taja:
Kumb.Na.NJBRRH/APP/01C/97

Wananchi wote,
TANZANIA.

KUH: TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA YA MKATABA.

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe inatangaza nafasi ya ajira ya mkataba kwa kada ya Mtekinolojia Maabara;-

MTEKINOLOJIA MAABARA "LABORATORY TECHNICIAN" NAFASI (2)

Sifa za Mwombaji

Kuajiriwa wenye Stashahada katika fani ya Uteknolojia Maabara kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na Baraza.

KAZI NA MAJUKUMU

- (i) Kupima sampuli zinazoletwa maabara.
- (ii) Kuhifadhi sampuli zinazotakiwa kufanyiwa uchunguzi au kupelekwa Maabara za ngazi za juu.
- (iii) Kufanya kazi za ukaguzi wa maabara, vitendanishi, vifaa, kemikali na hifadhi ya kemikali
- (iv) Kuweka kumbukumbu za maabara ambazo zimepatikana wakati wa uchunguzi.
- (v) Kufundisha watumishi walio chini yake.
- (vi) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

MASHARTI YA JUMLA.

1. Ngazi ya mshahara ya kila nafasi itazingatia mwongozo wa kitaifa uliotolewa Julai 2021 unaohusu namna ya kushughulika na malipo ya watumishi wa kujitolea kada za afya au jinsi itakavyoelekezwa na Katibu Mkuu Afya.

2. Mwombaji awe raia wa Tanzania mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi 45
3. Kila mwombaji anatakiwa aambatanishe nakala ya vyeti vya sekondari, taaluma na kuzaliwa na picha ndogo za rangi mbili za hivi karibuni "passport size" pamoja na wasifu binafsi unaoonesha namba za simu na anuani zake na za wadhamini watatu (3) wa uhakika.
4. Waombaji wanatakiwa wawe wamesajiliwa na Bodi la taaluma na waambatanishe vyeti vya usajiri.
5. Mwombaji aandike nje ya bahasha kada/kazi/nafasi anayoomba
6. Uwasilishwaji wa vyeti vya kugushi utachukuliwa hatua za kisheria.

JINSI YA KUTUMA MAOMBI

Maombi yawasilishwe/kutumwa kabla ya tarehe 07.02.2022 saa tisa kamili alasiri.

Maombi yote yatumwe kwa njia mojawapo kati ya zifautazo

1. kwa mkono; maombi yawasilishwe Ofisi ya masijala Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Njombe siku za kazi.
2. kwa njia ya barua pepe, muombaji atume "Scanned documents" kwenda; njomberrh@afya.go.tz

Barua za maombi zielekezwe kwa Mganga Mfawidhi kwa kutumia anuani

Mganga Mfawidhi,

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa,

S. L. P 1044

NJOMBE.

NB: Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe haihitaji mtuma maombi yoyote kutoa fedha katika hatua zote za ajira hii.

Tangazo hili limetolewa tarehe 31/01/2022 na



Hassan Majaliwa
Afisa Mawasiliano
Hospitali ya Rufaa ya Mkoa
NJOMBE.